# IDARA YA AFYA NA ELIMUSIHA YA KIAKILI YA MARYLAND NA MAELEZO YAKO YA AFYA

## ILANI YA MAADILI YA FARAGHA

**ILANI HII INAFAFANUA JINSI AMBAVYO MAELEZO YA AFYA KUKUHUSU YANAVYOWEZA KUTUMIWA NA KUFICHULIWA NA JINSI UNAVYOWEZA KUFIKIA MAELEZO HAYA. TAFADHALI HAKIKI KWA UANGALIFU.**

### Utangulizi

Idara ya Afya na Elimuisha ya Kiakili ya Maryland (DHMH) imejitolea kulinda maelezo yako ya afya. DHMH inahitajika kisheria kudumisha faragha ya Maelezo Yaliyolindwa ya Afya (PHI). PHI inajumuisha maelezo yoyote yanayotambulika tunayopata kutoka kwako au watu wengine yanayohusiana na afya yako ya kimwili na kiakili, huduma ya afya uliyopokea, au malipo kwa huduma ya afya. Kama inavyohitajika kisheria, ilani hii hukutolea maelezo kuhusu haki zako na majukumu yetu ya kisheria na maadili ya faragha kulingana na faragha ya PHI. Ili kutoa matibabu au kulipia huduma yako ya afya, DHMH itakuuliza baadhi ya maelezo ya afya na maelezo hayo ya afya yatawekwa kwenye rekodi yako. Kwa kawaida rekodi inajumuisha dalili, uchunguzi na matokeo yako ya jaribio, utambuzi, na matibabu. Maelezo hayo, yajulikanayo kama rekodi yako ya afya au matibabu, na yanayodhibitiwa kisheria kama maelezo ya afya, yanaweza kutumika kwa malengo mbalimbali. DHMH na Washiriki wake wa Biashara wanahitajika kufuata maadili ya faragha yaliyofafanuliwa kwenye Ilani hii, ingawaje DHMH inahifadhi haki ya kubadilisha maadili yetu ya faragha na masharti ya Ilani hii wakati wowote. Unaweza kuomba nakala ya Ilani mpya kutoka kwa wakala wowote wa DHMH. Pia imechapishwa kwenye tovuti yetu katika http://dhmh.maryland.gov.

### Matumizi na Ufichuzi Unaoruhusiwa

Waajiriwa wa DHMH watatumia maelezo yako ya afya tu wanapofanya kazi zao. Kwa matumizi mbali na yale DHMH hufanya kwa kawaida, lazima DHMH iwe na uidhinishaji wako katika maandishi isipokuwa iwapo sheria inaruhusu au inahitaji hivyo, na unaweza kukataa uidhinishaji kama huo kwa buraa ilio na kipimo. Ifuatayo ni baadhi ya mifano ya uwezekano wa matumizi yetu na ufichuzi wa maelezo yako ya afya:

**Matumizi na Ufichuzi bila Ridhaa Inayohusiana na Matibabu, Malipo, au Oparesheni za Huduma ya Afya:**

- **Kwa matibabu:** DHMH inaweza kutumia au kushiriki maelezo yako ya afya ili kuidhinisha, kukataa matibabu, na kuthibitisha iwapo matibabu yako yanafaa. Kwa mfano, Watoa huduma wa afya wa DHMH wanaweza kuhitaji kuhakiki matibabu yako na mtoa huduma wako wa afya kwa umuhimu wa matibabu au kwa uratibu wa huduma.
- **Ili kupata malipo:** DHMH inaweza kutumia na kushiriki maelezo yako ya afya ili kutoa bili na kukusanya malipo kwa huduma zako za afya na kutambua ustahiki wako kushiriki kwenye huduma zetu. Kwa mfano, mtoaji huduma wako wa afya anaweza kutuma malalamishi kwa malipo ya huduma za matibabu zilizotolewa kwako.
- **Kwa oparesheni za huduma ya afya:** DHMH inaweza kutumia au kushiriki maelezo yako ya afya ili kutathmini ubora wa huduma zinazotolewa, au kwa jimbo letu au wakaguzi wa hesabu wa shirikisho.

**Matumizi na Ufichuzi Mwingine wa Maelezo ya Afya Unaohitajika au Kuruhusiwa Kisheria:**

- **Malengo ya maelezo:** Isipokuwa utupe maagizo mbadala, DHMH inaweza kutuma vikumbusho vya miadi na nyenzo zingine kuhusu mpango nyumbani kwako.
- **Inahitajika kisheria:** DHMH inaweza kufichua maelezo ya afya wakati sheria inatuhitaji kufanya hivyo.
- **Shughuli za afya ya umma:** DHMH inaweza kufichua maelezo ya afya wakati DHMH inahitajika kukusanya au kuripoti maelezo kuhusu magonjwa, majeraha, au kuripoti takwimu muhimu kwa migawanyiko mingine katika idara na mashirika mengine ya afya ya umma.
- **Shughuli za uangalizi wa afya:** DHMH inaweza kufichua maelezo yako ya afya kwa migawanyiko mingine katika idara na wakala nyingine kwa shughuli za uangalizi inavyohitajika kisheria. Mifano ya shughuli hizi za uangalizi ni uhariri, ukaguzi, uchunguzi, na utoaji leseni.
- **Korona, Wachunguzi wa Matibabu, Wakurugenzi wa Matanga na Utoaji wa Viungo:** DHMH inaweza kufichua maelezo ya afya yanayohusiana na kifo cha korona, wachunguzi wa matibabu au wakurugenzi wa matanga, na kwa mashirika yaliyoidhinishwa yanayohusiana na utoaji wa viungo, jicho, au misuli au upandikizaji.
- **Malengo ya utafiti:** Kakita baadhi ya hali, na chini ya usimamizi wa Bodi yetu ya Uhakiki wa Kitaasisi au

bodi nyingine teule ya faragha, DHMH inaweza kufichua maelezo ya afya ili kusaidia utafiti wa matibabu.

- **Zuia vitisho kwa afya au usalama:** Ili kuzuia vitisho hatari kwa afya au usalama, DHMH inaweza kufichua maelezo yanayohitajika kwa utekelezaji wa sheria au watu wengine wanaoweza kuzuia au kutoa leseni kwenye vitisho vinavyodhuru.
- **Matumizi mabaya na utelekezaji:** DHMH itafichua maelezo yako ya afya kwa mashirika sahihi iwapo kwa kweli tutaamini kuwa unaweza kuwa mwathiriwa wa matumizi mabaya, kutelekezwa, vurugu ya nyumbani, au uhalifu mwingine unaowezekana. DHMH inaweza kufichua maelezo yako ya afya kwa umbali unaofaa kuzuia vitisho hatari kwa afya au usalama wako au afya au usalama wa wengine.
- **Kazi maalum za serikali:** DHMH inaweza kufichua maelezo ya afya ya mfanya kazi katika jeshi na maveterani katika hali fulani, kwa vifaa vya urekebishaji katika hali fulani, kwa programu za faida ya serikali na uandikishaji, na kwa sababu za usalama wa taifa, kama vile ulinzi wa Rais. .
- **Familia, marafiki, au watu wengine wanaojihusisha kwenye huduma yako:** DHMH inaweza kushiriki maelezo yako ya afya na watu kwa kuwa inahusiana moja kwa moja katika kujihusisha kwako kwenye huduma yako au malipo ya huduma yako. Pia DHMH inaweza kushiriki maelezo yako ya afya na watu ili kuwaarifu kuhusu eneo, hali ya kawaida, au kifo chako.
- **Fidia kwa wafanyakazi:** DHMN inaweza kufichua maelezo ya afya kwa mipango ya fidia kwa wafanyakazi inayotoa faida kwa majeraha yanayohusiana na kazi au magonjwa bila kujali kosa.
- **Saraka za wagonjwa:** Mashirika ya DHMH kwa kawaida hayatunzi saraka kwa ufichuzi kwa wapigaji simu au wageni wanaokuulizia kwa jina. Hata hivyo, iwapo shirika la DHMH linatunza saraka, hutatambuliwa kwa mpigaji simu au mgeni asiyejulikana bila uidhinisho, na maelezo yenye kipimo tunayofichua yanaweza kujumuisha jina lako, eneo katika shirika, hali yako ya kawaida (k.m., nzuri kiasi, thabiti, n.k.) na uhusiano wako wa kidini.
- **Kesi za kisheria, migogoro na madai:** Iwapo unahusishwa kwenye kesi ya kisheria, mgogoro, au madai, DHMH inaweza kufichua maelezo yako ya afya kwa mujibu wa mahakama au agizo la utawala, hati ya kuitwa mahakamani, ombi la ugunduzi, upelelezi wa madai yaliyowasilishwa mahakamani kwa niaba yako, au mchakato mwingine wa kisheria.
- **Utekelezaji wa sheria:** DHMH inaweza kufichua maelezo yako ya afya kwa afisa wa utekelezaji wa sheria kwa malengo ambayo yanahitajika kisheria au kwa majibu hati ya kuitwa mahakamani.
- **Watu wengine wa kutekeleza shughuli zinazoruhusiwa:** DHMH inaweza kuendesha shughuli zilizofafanuliwa hapo juu sisi wenyewe, au tunaweza kutumia mashirika yasiyo ya DHMH (yanayofahamika kama Washiriki wa Biashara) kutekeleza oparesheni hizo. Katika matukio hayo ambayo tunafichua PHI yako kwa mtu mwingine anayetenda kwa niaba yetu, tutalinda PHI yako kupitia makubaliano ya faragha yanayostahili.
- **Shughuli za Kuchangisha Pesa:** DHMH inaweza kutumia maelezo kukuhusu ili kuwasiliana nawe katika juhudi za kuchangisha pesa kwa DHMH na oparesheni zake. Maelezo tunayotoa kukuhusu yatakuwa na kipimo kwa maelezo yako ya mwasiliani, kama vile jina, anwani na nambari yako ya simu na tarehe ambazo unapokea matibabu au huduma katika DHMH.

## Haki Zako

**Una Haki ya:**

- **Kuomba uzuiaji:** Una haki ya kuomba uzuiaji au uwekaji kipimo kuhusu maelezo ya afya ambayo DHMH hutumia au hufichua kukuhusu. DHMH itashughulikia ombi lako ikiwezekana, lakini haihitajiki kisheria kukubali kizuizi kilichoombwa. Isipokuwa vinginevyo inavyohitajika kisheria, lazima DHMH ishughulikie ombi lako iwapo ufichuzi ni mpango wa afya kwa malengo ya kutekeleza malipo au oparesheni ya huduma ya afya (na sio kwa malengo ya kutekeleza matibabu); na maelezo ya afya yaliyolindwa ipasavyo tu kwa kipengee cha huduma ya afya au huduma ambayo mtoa huduma wa huduma ya afya anahusika imelipwa kikamilifu malipo ya kutoka kwenye mfuko.
- **Kuomba mawasiliano ya siri:** Una haki ya kuuliza DHMH ikutumie maelezo kwenye anwani mbadala au kwa mbinu mbadala. Lazima DHMH ikubali ombi lako almuradi tu ni rahisi kwetu kufanya hivyo.
- **Kukagua na kunakili:** Kwa baadhi ya vizuizi (kama vile madokezo ya matibabu ya kisaikolojia, maelezo yaliyokusanywa kwa vikao fulani vya kisheria, na maelezo ya afya yanayozuiwa kisheria), una haki ya kuona maelezo yako ya afya kulingana na ombi lako katika maandishi. Iwapo unataka nakala za maelezo yako ya afya, unaweza kutozwa ada inayoeleweka na inayolingana na gharama kwa kunakili, uchapishaji, na kuandaa ufafanuzi au muhtasari wa maelezo ya afya yaliyolindwa. Una haki ya kuchagua sehemu za maelezo yako unazotaka kunakili na kuwa  na maelezo ya kabla ya gharama za kunakili. Iwapo DHMH hutunza maelezo yako ya afya kwa kutumia rekodi za afya za kielektroniki, tutatoa ufikiaji katika umbizo la kielektroniki na kusambaza nakala za maelezo ya afya kwa shirika au mtu uliyemteu, alimradi chaguo lolote hilo liko wazi, linaonekana na maalum.

- **Kuomba marekebisho:** Unaweza kuomba katika maandishi kuwa DHMH irekebishe au iongeze kwenye rekodi yako ya afya. DHMH itajibu ombi lako baada ya siku 60, kwa hadi urefusho wa siku 30, iwapo unahitajika. DHMH inaweza kukataa ombi iwapo DHMH inatambua kuwa maelezo ya afya ni: (1) sahihi na kamilifu; (2) hayajaundwa na sisi na/au sio sehemu ya rekodi zetu; (3) hayaruhusiwi kufichuliwa. Iwapo DHMH itaidhinisha ombi kwa marekebisho, DHMH itabadilisha

  maelezo ya afya na kukujulisha, na DHMH itawaambia wengine ambao wanahitaji kujua kuhusu mabadiliko kwenye maelezo ya afya.
- **Kuhitaji uidhinishaji:** Una haki ya kuhitaji uidhinishaji wako kwa matumizi zaidi na ufichuzi wa madokezo ya matibabu ya kisaikolojia, kwa kupokea mawasiliano ya utangazaji na kwa mauzo ya PHI yako.
- **Kupokea uhasibu wa ufichuzi:** Una haki ya kuomba orodha ya ufichuzi iliyotengenezwa kwa maelezo yako ya afya baada ya Aprili 14, 2003, na kwa miaka sita kabla ya tarehe ambayo uhusibu umeombwa. Vizuizi na maelezo ya afya ambayo yametumiwa kwa matibabu, malipo, na oparesheni za huduma ya afya. Zaidi ya hayo, DHMH haifai kuorodhesha ufichuzi uliofanywa kwako, kulingana na uidhinishaji wako katika maandishi, uliotolewa kwa usalama wa taifa, kwa maafisa wa utekelezaji wa sheria, au vituo vya urekebishaji. Hakutakuwa na gharama kwa orodha kama hiyo kila mwaka. Kwa kuongezea, DHMH itatoa uhasibu wa ufichuzi uliotengenezwa kupitia rekodi ya afya ya kielektroniki ya matibabu, malipo, na oparesheni za huduma ya afya, lakini maelezo yamewekewa kipimo cha miaka mitatu kabla ya tarehe ya ombi.
- **Kuchagua Kutoka:** Una haki ya kupokea mawasiliano ya kuchangisha pesa na haki ya kuomba kuondoka kwenye mawasiliano ya kuchangisha pesa. Pia una haki ya kuchagua kutoka kwenye saraka ya mgonjwa ya kituo cha DHMH.
- **Kupokea ilani:** Una haki ya kupokea nakala ya karatasi ya Ilani hii na/au nakala ya kielektroniki kupitia barua unapoombwa.
- **Kupokea arifa za ukiukaji:** Una haki ya kupokea arifa kila wakati ukiukaji wa PHI yako isiyo salama hutokea.
- **Kupokea ulinzi wa maelezo ya kijenetiki:** Iwapo kijenzi chochote cha huduma ya afya cha DHMH kinazingatiwa kuwa mpango wa afya, mpango wa afya inapigwa marufuku kutumia au kufichua maelezo yako ya kijenetiki kwa baadhi ya malengo ya maandishi ya chini.
- **Kupokea ulinzi wa rekodi za afya ya akili:** Iwapo rekodi ya matibabu inayoundwa kulingana na upokeaji wako wa huduma za afya ya akili itafichuliwa bila shirika lako, DHMH itatoa tu maelezo kwenye rekodi ambayo ni muhimu kwa lengo ambalo ufichuzi umepangwa.

**Kwa Maelezo zaidi:**
Waraka huu unapatikana katika lugha nyingine na maumbizo mbadala yanayotimiza miongozo kwa Wamerika walio na Sheria ya Ulemavu. Iwapo una maswali yoyote na ungependa maelezo zaidi, unaweza kuwasiliana na: **(Ingiza Jina na Nambari ya Mwasiliani wa Faragha wa Kitengo Kilichoteuliwa cha Biashara)**________________________

**Ili Kuripoti tatizo kuhusu Maadili yetu ya Faragha:**
Iwapo unaamini kuwa haki zako za faragha zimekiukwa, unaweza wasilisha malalamiko.

- Unaweza kuwasilisha malalamiko kwa Idara ya Afya na Elimusiha ya Kiakili, Kitengo cha Uzingatiaji wa Shirika katika 1-866-770-7175.
- Unaweza kuwasilisha malalamiko kwa katibu wa Idara ya Marekani ya Huduma za Afya na Binadamu, Ofisi ya Haki za Kiraia Unaweza kupigia Idara ya Afya na Elimusiha ya Kiakili kwa maelezo zaidi.

DHMH haitachukua hatua yoyote ya kulipiza kisasi dhidi yako iwapo utatoa malalamiko hayo.
**Tarehe ye Kuanza kutumika:** Ilani hii ilianza kutumika Agosti 19, 2013.

---

**(Lazima programu za mtoa huduma zihakikishe kuwa zinajaribu kutia sahihi kwenye uthibitisho huu)**
Uthibitisho wa kupokea ilani hii:

________________________________ ____________________

Mgonjwa au Mwakilishi Aliyeidhinishwa Tarehe

Iwapo huwezi kupata uthibitisho, bainisha sababu:

______________________________________

Sahihi ya mwakilishi wa DHMH